# IDB GRADUATES ASSOCIATION OF TANZANIA

**KANUNI ZA KUDUMU ZA JUMUIYA YA WAHITIMU WALIODHAMINIWA NA BENKI YA MAENDELEO YA WAISLAM TANZANIA**

**ZIMETAYARISHWA NA KAMATI YA UTENDAJI YA IDB-GAT, NOVEMBA, 2020**
**ZIMEPITISHWA NA WANACHAMA WA IDB-GAT, DESEMBA, 2020**

## SEHEMU YA KWANZA

## UTANGULIZI

KWA KUWA kauli mbiu ya Jumuiya ni kuhakikisha Jamii inakuwa katika misingi inayozingatia utu, maadili mema, tamaduni zinazopendeza,uaminifu, wema, kusaidiana, kuondoa na kutokomeza uhalifu, rushwa, kutoaminiana, tabia za ulevi na kila aina ya tabia na matendo yasiyozingatia utu wa mwanadamu.

KWA KUWA uwepo wa Mmomonyoka wa maadili, watu kukosa wema, uadilifu, tabia za rushwa, ulevi na uhalifu katika jamii. Haya yote huchochewa na unajidhihirisha kwa kukithiri kwa umasikini, malezi mabaya ya familia, malezi ya mzazi mmoja ya watoto, watu kukata tamaa na watoto wa mitaani.

KWA KUWA Jumuiya inatambua kuwa jukumu la kuisimamia jamii na kurudisha utu wa mtu na thamani ya mwanadamu linahitaji jitihada za watu wenyewe na kwamba jukumu la kuirekebisha jamii si la Serikali peke yake bali ni la kila mwanajamii.

KWAHIVYO Jumuiya hii imeona kuna haja ya kuanzishwa kwa Jumuiya ya kujitolea katika kusaidia jamii zao, Mashirika yasiyo ya kiserikali au Jumuiya isiyokuwa ya kisiasa. Hivyo Jumuiya imeona kuanzishwa kwa Shirika lisilo la Kiserikali ili kuweza kutimiza malengo kama ilivyo taja hapo juu na katika Katiba yake.

NA KWA KUWA Madhumuni ya kanuni hizi za kudumu ni kuweka utaratibu wa namna Jumuiya hii itakavyoendesha mikutano na shughuli zake kwa kuzingatia misingi ya utawala bora.

SASA BASI Kanuni hizi za Kudumu zinaelekeza ifuatavyo:-

1. Kanuni hizi zitaitwa Kanuni za Kudumu za JUMUIYA YA WAHITIMU WALIODHAMINIWA NA BENKI YA MAENDELEO YA WAISLAMU TANZANIA, Toleo la kwanza Novemba, 2020.
2. Bila ya kuathiri masharti ya Katiba, Kanuni hizi zitatumika kwa mambo yote yanayohusu utaratibu wa uendeshaji wa Shughuli za Jumuiya.

*Iwapo jambo au shughuli yoyote haikuwekewa masharti katika Kanuni hizi, Mwenyekiti ataamua utaratibu wa kufuata katika jambo au shughuli hiyo, kwa kuzingatia Quran, Hadith, Ijitimai, Qiyas, Katiba, Sheria nyingine za nchi, Kanuni nyingine zilizopo, maamuzi ya awali ya wenyeviti wa Jumuiya pamoja na mila na desturi za kislamu za uendeshaji bora wa Shughuli za Juya na uamuzi huo utaingizwa katika Muhtasari wa Maamuzi ili kuongoza mwenendo wa baadaye wa uendeshaji wa Shughuli za Jumuiya.*

3. Katika Kanuni hizi, isipokuwa kama maelezo yatahitaji vinginevyo:-

“**Akidi**” ni idadi ya Wanajumuiya inayoruhusu kufanya maamuzi ya Jumuiya kwa mujibu wa Katiba kipengele namba sita (6) cha katiba ya Jumuiya hii;

“**Bodi**” ni Bodi ya Udhamini ya Jumuiya ya Wahitimu Waliodhaminiwa na Benki ya Maendeleo ya Waislamu Tanzania kwa mujibu wa Katiba kifungu namba 1.5.3;

"**Kamati ya Uendeshaji** " Kamati ya usimamizi wa kazi za Jumuiya inayoteulia na Mkutano mkuu wa mwaka kwa mujibu wa Katiba kifungu namba 1.5.4;

"**Kamati**" ni Kamati yoyote ya Jumuiya iliyoundwa kwa mujibu wa Katiba ya Jumuiya Ibara ya 6;

"**Jumuiya**" ni Jumuiya ya Wahitimu Waliodhaminiwa na Benki ya Maendeleo ya Waislamu Tanzania kwa mujibu wa Katiba kifungu namba 1.5.2;

"**Mwanajumuiya**" ni mtu yeyote mwenye sifa kwa mujibu wa Katiba kifungu namba 4.2 au 4.3 au 4.4

## SEHEMU YA PILI

## UENDESHAJI WA SHUGHULI ZA JUMUIYA

4. Mwenyekiti wa kamati ya uendeshaji na wasaidizi wake watachaguliwa na Wanachama kwa mujibu wa katiba ibara ya 4 ya kifungu kidogo cha 4.7 na kushika madaraka yao katika muda usiozidi vipindi viwili mfululizo kwenye nafasi moja.

5. Katika kutekeleza majukumu yao yaliyotajwa katika Ibara ya 6 ya Katiba, viongozi wataongozwa na Kanuni hizi na pale ambapo Kanuni hazikutoa mwongozo, basi viongozi watafanya kazi kwa kuzingatia Katiba, Sheria nyingine za nchi, Kanuni nyingine zilizopo, maamuzi ya awali ya viongozi wa Jumuiya pamoja na mila na desturi za Jumuiya nyengine zenye utaratibu wa kijumuiya unaofanana na utaratibu wa Jumuiya hii.

### Uchaguzi wa Viongozi

6. Taratibu za Uchaguzi wa Viongozi wa Jumuiya. Kwa kuzingatia masharti ya kanuni hizi viongozi watachaguliwa kwa kufuata utaratibu ufuatao.

(a) Kutakuwa na Uchaguzi wa viongozi utakaofanyika kwa mujibu wa masharti ya Ibara ya 4 kifungu kidogo cha 4.7 ya Katiba pamoja na Kanuni hizi.

(b) Kila mwanajumuiya atakuwa na haki ya kupendekeza majina ya viongozi ambao watakuwa wagombea wa nafasi za uongozi, kwa mujibu wa Katiba.

(c) Utakapofika wakati wa uchaguzi wanajumuiya (ambao sio viongozi) watapendekeza Majina matatu ya wanajumuiya (ambao sio viongozi) watakao simamia uchaguzi.

(d) Baada ya kupokea majina hayo, kamati ya kusimamia uchaguzi itayachambua na kisha itawasilisha majina ya wagombea wenye sifa kwa wanachama wote siku mbili kabla ya uchaguzi.

(e) Endapo wamependekezwa wagombea wawili au zaidi, uchaguzi utafanyika kwa kufuata utaratibu ulioainishwa katika fasili zinazofuata za Kanuni hii.

(f) Mgombea yeyote anaweza kuitaarifu kamati ya kusimamia uchaguzi kwa maandishi kwamba anajitoa kugombea, kabla ya shughuli za kupiga kura kuanza basi kamati italiondoa jina la mgombea huyo katika orodha ya wagombea.

(g) Kura zitapigwa kwa karatasi ama kwa mtandao, atakayeongoza kwa kura atashika nafasi husika na atakae mfuatia atakuwa msaidizi wake.

## SEHEMU YA TATU

## MIKUTANO NA VIKAO VYA JUMUIYA

7.-(1) Mkutano / kikao utafanyika mahali, tarehe na saa ambayo mwenyekiti/ katibu atatamka wakati akiitisha Mkutano husika.

(2) Bila ya kuathiri Masharti ya Kanuni hizi kuhusu kuanza na kufungwa kwa vikao vya Jumuiya, Mkutano/ kikao utaendelea kwa muda wowote ambao utahitajika kwa ajili ya kutekeleza na kukamilisha shughuli zote za Mkutano/kikao.

(3) Mwenyekiti ataongoza mkutano/kikao na Katibu ataratibu mkutano/kikao ikiwa ni pamoja na kuandika muhtasari. Mikutano/ vikao vyote vitaanza na kufungwa kwa dua.

(4) Endapo Mwenyekiti na Makamu wake hawapo, wanachama chini ya uongozi wa katibu watapendekeza jina la mwanajumuiya mmoja atakae kuwa mwenykiti wa muda wa mkutano/kikao husika.

## SEHEMU YA NNE

## SHUGHULI ZA JUMUIYA

8.-Bila kuathiri kifungu namba 2.2 cha Katiba Jumuiya hii itafanya shughuli zifuatazo:

(1) Kukusanya na kuratibu, michango, swadaka na zakka toka kwa watu na taasisi mbalimbali.

(2) Kuhamasisha, kushawishi na kuratibu upatikanaji wa rasilimali mbalimbali toka katika jamii kwa ajili ya kuendeleza elimu, teknolojia na afya.

(3) Kupanga na kuratibu miradi ya maendeleo ya ustawi wa jamii

(4) Kuratibu na Kushirikiana na taasisi nyingine zisizo za kiserikali za nje na ndani katika kuleta maendeleo ya jamii.

(5) Kuandaa na kufikisha taarifa kwa jamii kwa njia ya maandishi, Tehama, na mikutano

(6) Kulinda haki za wanachama kadri itakavyowezekana.

(7) Kuandaa na kutekeleza miradi kwa ajili ya kupata fedha za kuendeshea Jumuiya.

(8) Kusaidia wanachama na waislamu kujiendeleza kitaaluma ya dini na mazingira.

(9) Kuboresha uchumi, mahusiano na maendeleo ya Imani kwa jamii ya waislamu.

(10) Kufanya tafiti na kuandika vitabu kuhusiana na mwenendo wa uchumi.

## SEHEMU YA TANO

## KANUNI ZA MAJADILIANO

9. - Mwanajumuiya yeyote anaweza kumuarifu mwenyekiti kwa mdomo. ama maandishi ama simu, whatsApp nk hoja anayoiona ni muhimu ndani ya kikao au nje. Mwenyekiti baada ya kupata hoja husika atafanya yafuatayo:-

(1) Ataitisha kikao cha dharura kuhusu jambo husika au

(2) Atasubiri muda wa vikao vya kawaida na kuliweka jambo husika ndani ya agenda kwa ajili ya majadiliano

10. Wakati wa majadiliano mkutanoni au kwenye kamati yoyote , Mwanachama au kiongozi hatoruhusiwa kutumia lugha ya maudhi au ya matusi.

## SEHEMU YA SITA

## HAKI ZA MWANACHAMA

11. Mwanachama atakuwa na haki zifuatazo:-

1. Kutumia na kupata huduma zote za Jumuiya bila ubaguzi.
2. Kupokea taarifa ,kuona taarifa au kumbukumbu za Jumuiya kwa utaratibu unaokubalika wa taarifa husika.
3. Kuchagua (yaani kupiga kura) na kuchaguliwa (yaani kupigiwa kura) kwenye nafasi yoyote katika Jumiya kwa kuzingatia katiba na kanunu hizi
4. Haki ya kura moja kwa kila mwanajumuiya bila kujali kiasi cha michango aliyoweka kwenye Jumuiya.
5. Haki ya kujitetea dhidi ya jambo lolote litakalomkabili katika uhusiano wake na wanaJumuiya wengine.
6. Haki ya kutoa hoja yoyote inayohusu mwenendo wa wanajumuiya kwa kufuata taratibu

## SEHEMU YA SABA

## WAJIBU WA MWANAJUMUIYA

12. MwanaJumuiya atakuwa na wajibu ufuatao:-

1. Kuchangia fedha kila mwezi (ada) na michango mingine yoyote kama itakavyoanishwa kwenye kanuni au iliyopendekezwa na kuidhinishwa
2. Kuhudhuria na kushiriki katika mikutano yote halali ya Jumuiya.

3. Kuwa mtu Mwaminifu, Mwaadilifu, na Mwenye Kujitolea kwa ajili ya Jumuiya.

4. Kufuata kanuni, sheria na masharti ya kikundi yaliyo kubaliwa

5. Kutii na kufuata maazimio yote ya Mkutano wowote halali hata ikiwa hakuwepo kwenye mkutano huo, au kutoshiriki katika kupitisha azimio hilo

6. Kueneza sifa nzuri za Jumuiya

7. Kuwa na nidhamu wakati wa vikao au mikutano

8. Kushiriki kikamilifu kubuni miradi ya kuendeleza na kuimarisha Jumuiya

9. Kutunza siri zote za Jumuiya.

## SEHEMU YA NANE

## VYANZO VYA FEDHA

1. Ada za kila mwezi na swadaka mbalimbali.

2. Vitega uchumi mbalimbali (Investments), mashamba, Viwanja, biashara nk.

3. Mikopo kutoka vyombo vya fedha au chombo kingine chochote baada ya kupata idhini ya wanajumuiya kwa idadi ya theluthi mbili ya wanachama au Zaidi.

4. Misaada au Ufadhili kutoka sehemu mbalimbali.

5. Chanzo kingine chochote halali kwa mujibu wa sheria za nchi na katiba ya kikundi.